**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, ……………**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU –
TAMISEMI**

**Namba za Simu 0718004282**

**Mkuu wa Shule 0694188794**

**Makamu Mkuu wa Shule 0713306256**

**Makamu mkuu wa shule 0713740269**

**Matron/Patron 0715202700**

**Shule ya Sekondari MACECHU**

**S.L.P 5668 Tanga**

**Tarehe .................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………
……………………………………………..
S.L.P ……………………………………..
…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MACECHU HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA MKOA TANGA MWAKA ……………… KWA TAHASUSI ZA………………NA…………..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …………………na atasoma tahasusi ya……………………..

Shule ya Sekondari MACECHU ipo umbali wa Kilometa 10 Mashariki mwa Mji wa TANGA Usafiri wa basi kutoka mjini TANGA unapatikana katika kituo cha mabasi KANGE Nauli ni Shilingi 3000 kwa pikipiki na Shilingi 7000 kwa bajaji.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Mwanafunzi aje na za Sare ya shule ambayo ni suruali mbili za blue Bahari au kama itampendeza zinapatikana shule kupitia fundi wa shule kuepusha usumbufu kwa wanafunzi kutofautiana kimavazi shuleni gharama 18,000 kwa kila moja.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi;
iii. Sare ya Michezo ni trak suti moja na bukta moja rangi ya blue (Chelsea)
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta (dark blue) v-shape ;
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni suruali moja (nyeusi) na tisheti (nyeupe) aje akiwa amezivaa siku ya kuripoti. **Nguo za nyumbani haziruhusiwi**.
ix. Aje na Tisheti (T-shirt) ya kola rangi ya brauni yenye maandishi ya jina la shule au kama mzazi itampendeza inapatikana kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 12,000/=
x. Kila mwanafunzi anatakiwa Kuweka alama kwenye nguo na vifaa vyake alivyo navyo hapa shuleni au kama itampendeza shule inaweka alama kwenye nguo na vifaa vyote vya mwanafunzi kwa gharama ya tsh 10,000/=

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 12 ya counterbook (quare 3)
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka zinapatika katika duka la shule.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Begi jeusi la kubebea madaftar

v. Sanduku la bati (tranker). Mabegi ya aina nyingine hayaruhusiwi
vi. Dissecting Kit kwa wanafunzi wote
vii. Scientific Calculator, tochi na stop watch
viii. Godoro **jipya** kwa wanafunzi lenye refu futi 6, upana futi 2.5 na unene inchi 6;
ix. Mwanafunzi anatakiwa aje na Mashuka ya blue Bahari Jozi 2 au kama mzazi itampendeza Yanapatikana kwenye duka la shule kwa gharama ya Tsh 8,000/=kwa kila Moja
x. Foronya ya godoro 1, chandarua cha blue 1*;*
xi. Nguo za ndani za kutosha;
xii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xiii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xiv. Kwa wanafunzi wa mchepuo wa CBG waje na Kwanja 1, mopa moja, squiza moja, kwa mchepuo wa PCB waje na reki 1, mifagio 2 wa ndani (soft broom) na nje (wa chelewa)
xv. Unatakiwa uje na kopo lako la kuogea

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MICHANGO HII TU NDIYO IWEKWE KWENYE AKAUNT NAMBA 41701100103 NMB JINA- MKUU WA SHULE SHULE YA SEKONDARI MACECHU**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Kufeli, kutofanya mitihani au kupata alama “F” kwenye mitihani ya somo lolote na mazoezi darasani ni kosa lisilovumilika, utagharamia mitihani hiyo mwenye.
xiii. Nimarufuku mwanafunzi kubadili dini au kumshauri mwanafunzi mwenzake kubadili dini wanapokuwa shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi akikamatwa na simu hatua kali za kisheria zitachukuliwa.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**...............................................................**

**ABDALLAH R. KARATA**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0718004282**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0713 306 256**
- **Mwandamizi Taaluma 0714 146 737**
- **Mwandamizi Malezi 0713 740 269**

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI**
**ZA MITAA SHULE YA SEKONDARI MACECHU**
**S.L.P 5668**
**TANGA**

**FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA**

**SEHEMU A IJAZWE NA MWANAFUNZI**

| PICHA YA MWANAFUNZI |
|---|

1. Jina la mwanafunzi…………………………………………………………2. Uraia……………………….
3. Dini……………………………………….…4. Tarehe ya kuzaliwa ……………………..…..........
5.Shule uliyosoma kabla ya kuja MACECHU Sekondari……………………………………….
Sahihi ya mwanafunzi …………………………………………………………Tarehe……………………

**SEHEMU B: MAELEZO BINAFSI YA MZAZI /MLEZI**

| Picha ya Mzazi/Mlezi |
|---|

1.Jina kamili ………………………..…………………..……2. Anuani……………………………………
3.Wazazi wapo Hai /Wamefariki Baba /Mama. Anaishi na ……………………………………..
4.Wilaya ……………………..……….. Tarafa…………………………………..Kata………………………
Mtaa ……………………………………..Jina la M/kiti wa Mtaa ………………………………………
Anuani ya mwenyekiti wa mtaa…………………………………...........................................

4. Kazi unayofanya ……………………………………5. Namba ya simu :Baba/Mama……………………….

**SEHEMU C; KUKIRI**

Mimi ………………………………………mzazi /mlezi wa …………………………………………Nimesoma vyema sheria kanuni na taratibu za shule. Nakubali /Sikubali mwanangu ajiunge na shule ya Sekondari Macechu. Nitahakikisha kuwa mwanangu anapata mahitaji yote muhimu ya shule na kufuatilia kwa utaratibu maendeleo yake shuleni ya kitaaluma na nidhamu. Iwapo mwanangu atakwenda kinyume na sheria /taratibu za shule nakubali awajibishwe ipasavyo. Nitakuwa tayari muda wote kuitikia wito wa walimu na nitakuwa nikihudhuria vikao mimi mwenyewe.

Sahihi ya Mzazi /Mlezi…………………………..Tarehe ……………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………………….nakubali /sikubali nafasi niliyopewa katika shule ya Sekondari MACECHU.

Naahidi kuwa nitazitii kanuni na sheria zote za shule. Nitafuata masharti yote yatakayotolewa na Mkuu wa shule , Walimu na viongozi wote wa shule .

Naahidi pia kuwa nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo ili kuinua kiwango cha taaluma, mazingira safi na kukuza jina zuri la shule yetu ya MACECHU.

**…………………………………………..**

**Sahihi ya mwanafunzi**

**Tarehe ……………………………**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

MACECHU SEC. SCHOOL
P.O BOX 5668
**TANGA**

TO: MEDICAL OFFICER
…………………………………….
…………………………………….

**RE: MR/MISS (Full Name )…………………..…………………………………………………………………………….**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time schooling course. The examination should include the following categories (i –iii) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of a defect. Pregnancy (category iv) will also render a girl applicant ineligible for the course .

**(i)** (a) Eye - sight
(b) Hearing
(c ) Limbs
(d) Speech
(e) Venereal Diseases (s)
(f) Leprosy
(g) Epilepsy
**(ii)** Neurosis
**(iii)** Other serious diseases
**(iv)** Pregnancy

**Signature …………………………………………………….**

---

**PART B**

**MEDICAL CERTIFICATE**

**(**To be completed by Government Medical officer )

I have examine the above named and consider that he/she is physically fit/ unfit and mentally fit/ unfit for a full a time schooling course.

**i**. (a) Eye - sight ………………………………….(b) Hearing ………………………………………..
(c ) Limbs …………………………………………….(d) Speech………………………………………
(e) Veneral Diseases …………………………(f) Leprosy ……………………………………
(g) Epilepsy…………………………………………
**ii**. Neurosis…………………………………………………..
**iii**. Other serious diseases………………………………………..
**IV.** Pregnancy test ……………………………………………………

Signature………………………………………….
Station …………………………………………….. Designation……………………………………..
Date………………………………………………

## TAARIFA YA MAANDALIZI YA MAPOKEZI YA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO ………. NA MIKAKATI YA UFUNDISHAJI SHULE YA SEKONDARI MACECHU

Kwa mwaka ……… shule ya sekondari MACECHU imepangiwa wanafuzi …… kwa tahasusi mbili ambapo wanafunzi ……………watasoma…………..na ……. wengine watasoma…………..

**MIUNDOMBINU**

Maandalizi ya kuwapokea wanafuzi hawa yapo vizuri kwani bweni lililopo linatosha kwa idadi hiyo ya wanafunzi na vitanda vyote vipo katika hali nzuri,kwa sasa tunaendelea na ukarabati mdogo wa kubadilisha waya za kuzuia mbu madirishani pamoja na kuimarisha milango ya kwenye vyoo kazi ambayo hadi kufikia TAREHE…………… itakuwa imekamilika. Madarasa yote yapo katika hali nzuri na yana viti na meza zakutosha hivyo hakuna changamoto yoyote kwa upande wa miundo mbinu.

**UFUNDISHAJI**

Shule imejipanga kuanza ufundishaji tarehe ………… kwani tayari walimu wameshapangiwa vipindi na wanaendelea kujiandaa kwa ajili ya kuanza kufundisha tarehe tajwa hapo juu.Mgawanyo wa masomo kwa kidato cha tano ni kama ifuatavyo;-

| SOMO | MWALIMU |
|---|---|
| GENERAL STUDY | ELISA W KIOSO |
| BASIC APPLIED MATHEMATICS | ERICK C RUGAMALA |
| CHEMISTRY | NASSORO HALIDI MAGOGO |
| PHYSICS | RAMADHANI RAMADHANI |
| BIOLOGY | STEVEN JAMES |
| GEOGRAPHY | JOHNSON F DENGERA |

Pamoja na ufundishaji shule imejipanga kutoa mazoezi ya wiki ya kutosha kwa wanafunzi hao ili kuhakikisha wafasoma kwa bidii ili waweze kufanya vizuri kwenye mitihani ya taifa.